**Jina……………………………………………………………………** **Nambari...……....................**

Sahihi ya Mtahiniwa........................................

Tarehe: ……………….............

102/2

**KISWAHILI LUGHA**

Karatasi ya pili

**MUDA :SAA 2 ½**

Atika School

F r e e O n l i n e A c a d e m y

**Kiswahili**

Karatasi ya pili

**Saa: 2½**

**MAAGIZO:**

- *Andika* ***nambari yako ya usajili*** *na* ***jina lako*** *katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote.*
- *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu cha maswali.*

***KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE:-***

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

*Karatasi hii ina kurasa* ***8*** *zilizopigwa chapa.Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**UFAHAMU**

***Soma taarifa ifuatayo halafu ujibu maswali***

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili ya mahuluki ni kuielewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa ?Tunaweza kula demokrasia ? Ni dude gani hili lina kichwa au mkia peke yake ? Je demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya **mafalahi** ? kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. 'Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!' 'Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima. Hata Marekani na Ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama vimata na tanutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. <u>**Wanatupikia**</u> <u>**majungu**</u> kisha wakatoweka.Kuna demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya. Mkereketwa wa uafrika akachanganua

Demokrasia ya Afrika basi imefuata mkondo huu wa umwagaji damu. Kila kukijiri uchaguzi zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutafuta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde.

Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu ati . Hali hii imesababisha maafa makubwa , uharibifu mkubwa wa mali, majeraha , ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake,kuzagaa kwa magonjwa ainati , uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha chochote kutokana na hali. Huku mataifa mengi Ulayani na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyingine kimaendeleo. Afrika imedumaa tu imesalia kuimba ule wimbo wake wa kutokea azali. 'Tutaendelea vipi na tunadhulumiwa na kaka wakubwa' Siasa za demokrasia katika bara la Afrika ina tija kubwa hususan kwa wale wachache wanaofanikiwa kuthibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. Ulitima wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi ambao hutumiwa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena. Demokrasia ya kweli imo mikononi mwa umma pale utakapojikomboa kimawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora, Uajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii uliosisiwa na Jean Jaeques Rousseau.

**MASWALI**

(a) Binadamu amechanganyikiwa kwa njia ipi? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Ni vipi Demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(c) Kwa nini inasemekana kuwa 'Demokrasia ni mchezo wa mizengwe?' (alama2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(d) Ni athari gani hutokana na kinyang'anyiro cha Demokrasia? (Alam 4)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(e) 'Dhiki za raia zimesalia kuwa mradi – hewa wa wanasiasa.' Eleza (Alama2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(f) Fafanua maana ya maneno na mafungu yafuatayo jinsi yalivyotumika katika taarifa (Alama3)

(i) Mafalahi

……………………………………………………………………………………………………

(ii) Wanatupikia majunga

……………………………………………………………………………………………………

(iii) Ukarabati

……………………………………………………………………………………………………

**MUHTASARI (ALAMA 15)**

ASKARI : Wapi leseni yako?

DEREVA : Mama nili….

ASKARI : Mama ulimwacha nyumbani ! Hapa tuko kazini. Mbona huna leseni ?

DEREVA : Nili….. eeh..

ASKARI : Kwa nini unabeba abiria kupita kiasi ?

DEREVA : Afande….

ASKARI : Afande kitu gain? Mbona magurudumu yako yamechakaa? Tazama kioo chako kimepasuka. Lete leseni haraka! (anapandisha hasira)

DEREVA : Nisamahe ofisa.

ASKARI : Njoo hapa haraka !(akisonga mbali na gari upande wa nyuma. Dereva anavuta kofia na kumwendea huku amefumbata kitu mkononi. Baada ya muda mfupi dereva anarudi huku akichekacheka. Gari linaondoka huku abiria wakitazamana na kutabasamu)

ABIRIA1 : (kwa dereva)Tulikwambia usibebe watu kupita kiasi. Unaona sasa?

DEREVA : Msijali. Lazima askari wapate mnofu nami nipate mchuzi wangu

ABIRIA1 : Kumbe huna leseni ya gari? Hata bima huna?

DEREVA : Mwenye gari anasema bima ni ghali.

ASKARI : Na kwa nini hukushtakiwa ?

DEREVA : Mimi ? Aah haiwezekani. Polisi wana njaa. Huyu nimemwachia shilingi mia moja.

ABIRIAII : Si utengeneze tu gari basi ?

**DEREVA : Polisi wanamaliza pesa. Kila mkondo na kituo unalipa. Kuna wale wa pesa kidogo. Ukisimamishwa na vigogo wenyewe waweza kulipa hata mia tano.**

**ABIRIAI : Kwa nini msisusie kuwapa?**

**DEREVA : Mtindo ndio huu. Mkono mtupu haulambwi. Gari lolote la abiria lazima litoe. Hata gari likiwa jipya na lina kila kitu, upende usipende utatoa.usipotoa utasingiziwa makosa kama vile kusafirisha bangi.**

**ABIRIAII : Na pesa zote hizo polisi wanazipeleka wapi ?**

**DEREVA : Hata wakubwa hupelekewa. Wana mgao wao. Tusipopunguza ada ya bima na kuwalipa polisi mshahara mzuri tatizo hili litaendelea kuwepo.**

**Maswali**

(a) Dondoa makosa yanayofanywa na madereva na polisi kwa kuzingatia sehemu ambayo haijakolezwa wino kifunguni. ( maneno 50 -55) (alama 7)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(b) Fupisha sehemu iliyokolezwa wino katika kifungu hiki. (maneno 60 - 65) (alama 6)

**Matayarisho**.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

**MATIMIZI YA LUGHA**

(a) Toa mfano wa neno lenye muundo wa silabi ya konsonanti tatu mwambatano pamoja na irabu (Alama1)

…………………………………………………………………………………………………………

(b) (i) Toa mfano wa sauti nazali (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………

(ii) Taja sauti mbili ambazo ni vikwamizo na hutamkiwa kwenye ufizi (Alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………

(c)Yakinisha sentensi hii; (alama 1)

Mgeni asipofika mama haandai chakula

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

(d) Ukizingatia neno lililo katika mabano, andika sentensi hizi katika hali ya kutendeka.

(i) Daraja hili (vuka) tu wakati wa kiangazi (Alama1)

……………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………….

(ii) Kitabu hicho (soma) ijapokuwa sura zingine hazimo (alama1)

…………………………………………………………………………………………………………

(e) Andika katika ukubwa wingi (alama 2)

Kitoto kijeuri kikiletwa kitarejeshwa kwao

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

(f)Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatayo

(i)Nafsi viambata

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

(ii) Nafsi huru

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

(g) Tunga sentensi ya neno moja yenye visehemu vifuatavyo vya sarufi (alama 3 )

(i) Kiambishi kiwakilishi cha kiima

(ii) Kiambishi kiwakilishi cha wakati uliopo

(iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendewa / mtendewa

(iv) Shina la kitenzi

(v) Kiambishi cha kauli ya kutendesha

(vi) Kiishio

(h) Unda nomino kutokana na mizizi ifuatayo (alama 2)

(i)–nyw-

……………………………………………………………………………………………………….

(ii) –f-

……………………………………………………………………………………………………….

(i) Andika maana mbili zinazojitokezea katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Alikuja kutupa watoto

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

(j) Huku ukitoa mifano miwili eleza matumizi ya kistari kifupi (alama3)

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(k) Tofautisha tungo zifuatazo:- (alama2)

a. Mtoto apigwaye ni mkorofi

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

b. Mtoto aliyepigwa ni mkorofi

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(l) (i) Mofimu ni nini? (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

(ii) Bainisha majukumu ya mofimu tofauti katika tungo lifuatalo :- (alama2)

'Atamaliza'

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

(m) Changanua sentensi hii ukutumia vielezo matawi (alama 4)

Daktari yule hulewa sana japo wateja wake humsifu sana.

(n) Tunga sentensi moja na uonyeshe sehemu zifuatazo kwa kupiga mstari (alama3)

a. shamirisho kipozi
b. shamirisho kitondo
c. shamirisho ala

(o)Bainisha matumizi ya **kwa** katika sentensi hizi (alama 2)

(i) Alienda kwao jana jioni

…………………………………………………………………………………………………………..

(ii) Vijana kwa wazee huambukizwa ugonjwa wa ukimwi

…………………………………………………………………………………………………………

(p)Tunga sentensi ukitumia neno ‘ila’ kama (alama 2)

(i) Nomino

…………………………………………………………………………………………………………

(ii) Kiunganishi

…………………………………………………………………………………………………………

q). Onyesha aina za vishazi katika sentensi ifuatayo (alama2)

Mkulima alipoenda shambani, alivuna mazao.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**Isimu jamii (alama 10)**

Katika dakika za mwanzo, mapapa hao walikuwa wanaonekana kulemewa na bahari iliyowazunguka. Ghafla kipenga kikapulizwa.kila samaki akatandaza pezi lake tayari kwa vita. Milio ya ‘Twende Nguru! Kazana paa tupae!’ ikahanikiza hewani. Mwishowe Musa aliwanyamazisha wapinzani kwa bao safi japo walidai alikuwa kajenga kibanda katika ardhi ya wenyewe. ‘That is it!’ alisikika kocha wa paa akisema huku karusha mikono hewani.

(a) Taja sajili inayorejelewa katika dondoo hili (alama 2)

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

(b) Thibitisha jibu lako kwa kutambua sifa tatu katika dondoo (alama 8)

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**KISWAHILI KARATASI YA 2**

**LUGHA**

**MTIHANI WA MWIGO WILAYA YA NYANDO**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. UFAHAMU**

a) Kutolewa dhana ya demokrasia na kuishia katika maswali yasiyo na majibu(2X1=alama2)
b) Umma utakapojikomboa kimawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora uajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii(2X1=alama2)
c) Walio madarakani hawataki kubanduka hutafutavisababu vya kukwepa wimbi la ushinde(2X1=alama2)
d) Husababisha maafa makubwa uharibifu mkubwa wa mali majeraha ukimbizi wa raia dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa na uhasama wa kikabila (4X1=alama4)
e) Ulitima wa umma hutumiwa na wanasiasa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena (2X1=alama2)
f) i) Wale wanaojifaidi kutokana na jasho lao kwa mfano wakulima,
ii) kutoa habari ya uongo au kudanganya
iii) kutengeneza kilichochakaa au **harbika** (3X1=alama3)

adhibu sarufi hadi makosa $12x^1/_2$ = alama 6

hijai hadi makosa $6x^1/_2$ = alama 3

*kosa la sarufi ni hadi nusu ya alama za mwanafunzi katika sehemu moja*

**UFUPISHO**

**MAKOSA YANAYOFANYWA NA DEREVA NA POLISI**

a)- Dereva kuendesha gari bila leseni

i. Kubeba abiria kupita kiasi
ii. Dereva kuendesha gari ambalo magurudumu yake yamechakaa
iii. Dereva kuendesha gari ambalo kioo limepasuka
iv. Dereva kuendesha gari ambalo halina bima
v. Polisi kupokea hongo wanayopewa na dereva
vi. Dereva kutoa hongo inayopokelewa na polisi (7x1=alama 7)

Utiririko alama 1

b)Dereva kulipa kila mkondo wanaoenda na kituo wanachokipitia

a) Polisi wa vyeo vya chini vilevile hupokea hongo
b) Magari yote ya abiria hutozwa malipo na polisi hata kama ni jipya na lina kila kitu
c) Polisi kusingizia madereva makosa wasiokuwa nayo
d) Polisi wanafaa kulipwa mshahara mzuri ili kupunguza ufisadi
e) Ada ya bima hasa magari ya abiria inafaa kupunguzwa (6x1=alama 6)

Utiririko alama 1

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) i) kkkI

mbwa/mbweha/(1x1=alama 1)

b) i)/m/,/n/ /ny/ /ng‘/(1x1=alama 1)

(ii) /s/, /z/ ($2x^1/_2$= alama 1)

c)mgeni akfika mama ataanda chakula (1x2=alama 2)

d) i) huvukika

ii)kinasomeka/husomeka (2x1=alama 2)

e) majitoto/matoto jeuri/majeuri yakiletwa yatarejeshwa kwao (1x2=alama 2)

*(lazima sentensi iwe moja katika ukubwa na wingi)*

f) i)Nimechoka-Tumechoka
Umechoka-Mumechoka
Amechoka-Wamechoka
ii) mimi/sisi
wewe/nyinyi
yeye/wao

g) Anamlisha/
ninamlevya (1x3=alama 3)

h) i)kinywaji/kinywa/kinywa (1x1=alama 1)
ii)kifo/mfo/kufa (1x1=alama 1)

i) Alitetea watoto
Alirusha watoto na kutoweka (2x1=alama 2)

j)
i. Uandishi wa tarehe(lazima mwanafunzi atunge sentensi)
ii. Kuonyesha nafasi ya viambishi katika neno kwa mfano viambishi vya ngeli
iii. Kuonyesha kuwa neno fulani nimofimu tegemezi
iv. Kutenganisha silabi za neno
v. Kuonyesha kuwa limeendelezwa kwa mstari ufuatao (zozote 3x1=alama 3)

k) o-rejeshi tamati kurejelea hali ya mazoea au wakati wowote (1x1=alama1)

o-rejeshi ya kati kurejelea wakati maluum (1x1=alama 1)

I)ni sehemu ya neno iliyo na maana fulani 2x1 (alama 2)

ii) A –Nafsi

ta –wakati ujao

m-mtendewa

li-mzizi

z-mnyambuliko

a-kimalizio/kiishio($6x^1/_3$=alama 2)

m) mwalimu huyu hufundisha vizuri ndiposa wanafunzi wake hupita vizuri((4x1=alama 4)

n)mama alimpikia baba chakula kwa gesi

kitendo kipozi ala (1x3=alama 3)

o) i) kielezi cha mahali

ii)pamoja na (1x2=alama 2)

p) kazi yake haina ila(dosari)

sote tulienda kanisani ila mama (1x2=alama 2)

q) Mkulima alipoenda shambani-tegemezi (1x1=alama1)

alivua mazao - huru (1x1=alama 1)

**ISIMUJAMII**

a)sajili ya michezo/uwanjani (1x2=alama 2)

b)sifa za sajili hii

i. lugha ya mafumbo/jazanda(kajenga kibanda..)
ii. lugha changamfu
iii. msamiati teule wa michezo kwa mfano kipenga bao
iv. uradidi/urudiaji
v. kuhamisha msimbo(that is it !)
vi. sentensi fupi fupi kwa mfano(ghafla kipenga kikapulizwa…) ( zozote 4x2=alama8)

*makosa ya hijai na sarufi yaadhibiwe*

